JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA NA OKTOBA, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2024 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi ikiambatana na hali ya joto nyakati za mchana, na kusababisha usumbufu kwa shughuli zinazofanywa maeneo ya wazi. Aidha, mwezi Oktoba, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache na kuashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli, hususan kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hali hii ilisababisha ongezeko kidogo la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho kwa maeneo machache. Aidha, mtawanyiko wa mvua hizo haukuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, kati mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya maziwa makuu. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2024.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Septemba, 2024


Katika kipindi cha mwezi Septemba 2024, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan maeneo ya ziwa Victoria. Aidha, katika kipindi hiki hakuna vipindi vya mvua kubwa vilivyojitokeza nchini. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 37.5 ndani ya saa 24 kilipimwa katika kituo cha Mwanza mnamo tarehe 30 Septemba, 2024.

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Septemba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2024 maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi yaliendelea kupata vipindi vya baridi. Kiwango kidogo zaidi cha joto la chini cha nyuzi joto 6.4 °C kilirekodiwa katika kituo cha Uyole kilichop mkoa wa Mbeya mnamo tarehe 4 Septemba, 2024. Katika kipindi hiki maeneo ya Uyole na Igeri yaliendelea kuwa na hali ya baridi ambapo viwango vya joto la chini vilishuka zaidi ya nyuzi joto 10 °C. Hali hii inaonesha mwendelezo wa hali ya baridi katika maeneo hayo ukilinganisha na maeneo mengine ya `nchi.

Kielelezo cha 1 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku katika mwezi Septemba, 2024 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Uchambuzi unaonesha kuwa, hali ya baridi iliendelea kujitokeza katika wiki ya kwanza ya Septemba, huku hali ya joto ikiongezeka taratibu katika wiki ya pili na kubadilika badilika kuelekea mwishoni mwa mwezi. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vinaonesha vipindi vya baridi vilijitokeza

zaidi katika maeneo ya Igeri ukilinganisha na Uyole, ambapo siku 20 kiwango cha joto kilikuwa nyuzi 10 °C au chini zaidi wakati Uyole ilirekodi siku 7 zenye joto kiwango hicho.




**Kielelzo 1.** Viwango vya joto la chini katika kituo cha Uyole na Igeri kwa mwezi Septemba, 2024.

Kwa upande wa viwango vya juu vya joto, hali ya joto zaidi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo hususan magharibi mwa nchi. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.8 °C kilirekodiwa katika kituo cha Tumbi kilichopo mkoani Tabora mnamo tarehe 26 Septema, 2024 ikifuatiwa na Mpanda (Mkoa wa Tabora), kilirekodi nyuzi joto 35.7 °C mnamo tarhe 27 na 28 Septemba, 2024. Aidha, hali ya joto ilijitokeza zaidi Mpanda (mkoa wa Katavi) ambapo kwa siku 9 viwango vya joto la juu vilikuwa nyuzi joto 35°C au zaidi.

**Jedwali 1**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Septemba, 2024


| Kanda | Kituo | Idadi ya Siku | Kiwango cha Joto la Juu ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Magharibi | Mpanda | 9 | ≥ 35 °C |
| | Tumbi | 6 | ≥ 35 °C |
| | Tabora | 1 | ≥ 35 °C |

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Septemba, 2024

Katika mwezi huu, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa na baadhi ya nyakati kufikia kilomita 60 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini yakiwemo ya ukanda wa pwani (Mikoa ya Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), maeneo ya kati mwa nchi (Singida na Dodoma), magharibi (Tabora) na nyanda za juu kusini magharibi (Songwe). Mnamo tarehe 10 Septemba, 2024 upepo mkali wenye kasi ya kilomita 60 kwa saa ulirekodiwa katika kituo cha Songwe. Vipindi vya upepo mkali vilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo. Ongezeko la vumbi na kupeperushwa takataka kulijitokeza na kusabisha kupungua kwa uono na kuathiri ubora wa hewa. Maeneo ya mwambao wa pwani yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa ya bahari na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini, ikiwemo usafiri sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika mwambao.

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2024 vipindi vya mvua vilivyoashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani na ziwa Victoria. Aidha, vipindi vichache vya mvua kubwa vilijitokeza nchini. Mnamo tarehe 17 Oktoba, 2024 kituo cha Mwanza Marine kilichopo mkoani Mwanza kilipima milimita 107.3 za mvua kwa saa 24 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kwa mwezi Oktoba, 2024 ikifuatiwa na kituo cha hali ya hewa Mwanza kilichopima milimita 100.0 siku hiyohiyo. Kituo cha Tumbi kilichopo mkoa wa Tabora kilipima milimita 68.8 tarehe 19 Oktoba. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 2.




**Kielelezo 2:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Oktoba, 2024


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**1.5 Hali joto kwa mwezi Oktoba, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2024, vipindi vichache vya baridi vilijitokeza kwa nyakati za usiku hususan katika mikoa ya Mbeya na Njombe. Kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 8.8 °C kiliripotiwa katika kituo cha Igeri (Mkoa wa Njombe) mnamo tarehe 6 Oktoba, 2024. Kwa upande mwingine, viwango vya juu vya joto viliripotiwa katika baadhi ya maeneo, hususan mikoa ya magharibi (Katavi na Tabora) pamoja na mikoa ya Morogoro na Kilimanjaro. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 35.9 kilirikodiwa katika kituo cha Ilonga mnamo tarehe 29 Oktoba, 2024.

**Jedwali 2**. Idadi ya siku ambazo viwango vikubwa vya joto la juu vilijitokeza kwa mwezi Oktoba, 2024

| Kanda | Kituo | Idadi ya Siku | Kiwango cha Joto la Juu ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| Pwani ya Kaskazini | Ilonga | 3 | ≥ 35 °C |
| | Morogoro | 1 | ≥ 35 °C |
| Magharibi | Mpanda | 2 | ≥ 35 °C |
| | Tumbi | 4 | ≥ 35 °C |
| Nyanda za juu kaskazini mashariki | Moshi | 2 | ≥ 35 °C |

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Oktoba, 2024**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), kati mwa nchi (Singida na Dodoma), magharibi (Tabora), nyanda za juu kusini magharibi (Songwe) pamoja na ziwa Victoria (Mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga). Mnamo tarehe 3 Oktoba 2024, kituo cha shinyanga kiliripoti upepo mkali unaofikia kilomita 60 kwa saa. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 11 Novemba, 2024*

**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz